TANGAZO LA SERIKALI Na. 799 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA USIMAMIZI NA TOZO YA USHURU,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MAWILI YANAYOINGIZWA NCHINI NA SHIRIKA LA WAKIMBIZI DUNIANI YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Mawili Yanayoingizwa Nchini na Shirika la Wakimbizi Duniani ya Mwaka 2023, na iatchukuliwa kuwa imeanza kutumika tangu tarehe 29 Septemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari mawili yaliyoainishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Shirika la Wakimbizi Duniani kmesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 29 Machi, 2024

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAGARI

| SN | Transport PO #/GPO # | Maelezo | Mwaka | Namba ya Injini | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 66161 | Toyota Coster Bus W/cooler, 29 seats, high roof, 4.2 diesel, model HZB70R – ZGMSS-P1 | 2023 | 1HZ-1055797 | 01 | JTGABCB8706720365 | limeingizwa |
| 2 | 66161 | Toyota Coster Bus W/cooler, 29 seats, high roof, 4.2 diesel, model HZB70R – ZGMSS-P1 | 2023 | 1HZ-1054622 | 01 | JTGABCB8X06720358 | limeingizwa |

Dodoma,
3 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*